
**SINGIDA YETU**
*NURU YA MAENDELEO*



Jarida Maalum la Maadhimisho ya Siku ya

# Wanawake DUNIANI 2026

MKOA WA SINGIDA




TOLEO LA MWEZI **MACHI 2026**

Pata nalala ya jarida hili na mengine kupitia **www.singida.go.tz**

# UTANGULIZI

## MAONI YA MHARIRI

*Toleo hili maalum la SINGIDA YETU linakuja katika kipindi muhimu ambacho dunia inaendelea kutathmini nafasi ya mwanamke katika maendeleo ya jamii. Siku ya Wanawake Duniani si tukio la maadhimisho pekee, bali ni kioo kinachoakisi hatua tulizopiga na kazi kubwa iliyobaki mbele yetu.*

*Katika zama hizi za mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, nafasi ya mwanamke imeendelea kujitokeza kwa nguvu mpya, siyo tena kama mshiriki wa pembeni, bali kama mhimili mkuu wa maendeleo jumuishi.*

*Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka 2026 yanaleta tafakari pana juu ya safari ya usawa wa kijinsia, tulipotoka, tulipo na tunapokwenda. Mkoa wa Singida umechukua hatua za mfano kwa kupeleka maadhimisho haya karibu zaidi na wananchi, kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa.*

*Hatua hii ina maana kubwa. Inaondoa dhana kwamba maendeleo ni ya wachache na badala yake inaleta ukweli kwamba kila mwanamke, bila kujali nafasi yake anastahili kushiriki na kunufaika.*

*Lakini pia, kuna ujumbe wa kina zaidi unaojitokeza: uwezeshaji wa wanawake haupaswi kuwa tukio la msimu bali ni mchakato endelevu. Mikopo, elimu, huduma za afya, msaada wa kisheria na fursa za kiuchumi ni nguzo zinazopaswa kuimarishwa kila siku.*

*Tunapoangalia Dira ya Taifa ya 2050, ni wazi kuwa hatuwezi kufika bila mchango sawa wa wanawake na wanaume. Hivyo basi, wajibu huu si wa serikali pekee, bali ni wa jamii nzima, kuanzia familia, taasisi hadi sekta binafsi.*

*Kama wahariri, tunaamini kuwa simulizi za wanawake wa Singida zinapaswa kusimuliwa, kusikika na kupewa nafasi. Ndani ya kila mwanamke kuna hadithi ya uthubutu, mapambano na mafanikio inayoweza kuhamasisha kizazi kizima.*

*Huu ni wakati wa kuchukua hatua.*
*Huu ni wakati wa kusimama pamoja.*
*Huu ni wakati wa kujenga mustakabali wenye usawa.*

*"Tunachochea Mendeleo, Kupitia Taarifa Sahihi"*



**Glory Kimaro**
Mhariri/Chief Editor

# UONGOZI MKOA WA SINGIDA



**MHE. HALIMA DENDEGO**
MKUU WA MKOA WA SINGIDA



**DKT. FATUMA MGANGA**
KATIBU TAWALA MKOA WA SINGIDA



**MHE. GODWIN GONDWE**
MKUU WA WLAYA YA SINGIDA



**DKT. VINCENT MASHINJI**
MKUU WA WLAYA YA MANYONI



**MHE. MOSES MACHALI**
MKUU WA WLAYA YA MKALAMA



**MHE. THOMAS APSON**
MKUU WA WLAYA YA IKUNGI



**MHE. SULEMAN MWENDA**
MKUU WA WLAYA YA IRAMBA

# YALIYOMO

**Uzinduzi wa Maadhimisho ya Wanawake ya Kipekee 2026!**
Mkoa wa SIngida - RC Dendego



**WILAYA YA MANYONI:**
Sauti ya Mwanamke wa Singida Safari ya Mabadiliko Inaendelea




**WILAYA YA IKUNGI:**
Wanawake ni Nguzo ya Uchumi wa Kisasa wa Taifa



**WILAYA YA SINGIDA**
Malezi, Maadili na Mustakabali wa Jamii



**WILAYA YA MKALAMA:**
Mwanamke Hasubiri Tena, Anachukua Hatua!



**WILAYA YA IRAMBA:**
Mwanamke: Jasiri, Mwenye Maono na Tayari kwa Mafanikio



**SIKU YA KILELE IRAMBA:**
"Malezi Bora, Maadili Imara"
Wito wa Mama Salma Kikwete



**MATENDO YA HURUMA:**
Wanawake wa Singida Wagusa Maisha ya Watoto Wenye Mahitaji



## SALAM ZA MKUU WA MKOA WA SINGIDA



*Ni kwa heshima na furaha kubwa kuwakaribisha kusoma toleo hili maalum la jarida letu la* **SINGIDA YETU**, *lililoandaliwa mahsusi kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2026 katika Mkoa wa Singida.*

*Maadhimisho haya ni fursa muhimu kwa jamii yetu kutafakari mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha usawa wa kijinsia, pamoja na kutathmini changamoto zilizopo na kuweka mikakati madhubuti ya kusonga mbele. Aidha, ni jukwaa la kuenzi mchango mkubwa wa wanawake katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ndani ya mkoa wetu na taifa kwa ujumla.*

*Katika maadhimisho ya mwaka huu, yenye kaulimbiu isemayo:*
***"Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana ni Msingi Jumuishi kufikia Dira ya Taifa ya 2050."***
*Kaulimbiu hii inatukumbusha kuwa maendeleo endelevu hayawezi kufikiwa bila kuhakikisha ushiriki kamili na wenye usawa wa wanawake na wasichana katika nyanja zote za maisha.*

*Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuhakikisha wanawake wanapata fursa sawa katika elimu, ajira, ujasiriamali na uongozi. Mkoa wa Singida umeendelea kuchukua hatua madhubuti katika kuwawezesha wanawake kupitia mikopo, mafunzo na majukwaa mbalimbali ya maendeleo, ili kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika uchumi.*

*Ninawahimiza wazazi na walezi kuwekeza zaidi katika elimu ya mtoto wa kike, kwani hiyo ndiyo njia ya uhakika ya kujenga jamii yenye usawa, maarifa na ustawi wa kudumu.*

*Aidha, tuendelee kushirikiana wanawake na wanaume katika kujenga jamii yenye haki na usawa kwa wote.*

*Hii ni fursa ya kujifunza, kuungana na kunufaika na huduma mbalimbali zinazotolewa ndani ya Mkoa wa Singida.*

*Kwa pamoja, tunaweza kuijenga Singida yenye usawa, maendeleo na matumaini kwa vizazi vijavyo.*

*Asanteni sana.*

**Mhe. Halima Dendego**
Mkuu wa Mkoa wa Singida



# 'MAADHIMISHO YA WANAWAKE YA KIPEKEE SINGIDA 2026' RC DENDEGO

## MKUTANO NA WAANDISHI WA HABARI



*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, katika mkutano na waandishi wa Habari akizungumza kuelekea ufunguzi wa Wiki la Siku ya Wanawake ngazi ya katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida.* | PICHA: GCU RS SINGIDA

**28 Februari, 2026**

Mkoa wa Singida ulianza rasmi maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2026 kupitia mkutano wa waandishi wa habari ulioitishwa na Mkuu wa Mkoa, Mhe. Halima Dendego, tarehe 28 Februari 2026 katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Akizungumza na wanahabari, Mhe. Dendego alitoa taarifa rasmi kwa umma kuhusu mwelekeo wa maandalizi na utekelezaji wa maadhimisho hayo, akisisitiza umuhimu wake katika kuendeleza ajenda ya usawa wa kijinsia, haki za wanawake, na uwezeshaji wa wanawake na wasichana.

Ushiriki wa Taifa katika Agenda ya Kimataifa
Katika maelezo yake, RC Dendego alibainisha kuwa Tanzania itaungana na mataifa mengine wanachama wa Umoja wa Mataifa kuadhimisha siku hiyo tarehe 8 Machi 2026, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mikataba, maazimio na itifaki za kimataifa na kikanda zinazohusu maendeleo ya wanawake.

Alieleza kuwa Serikali tayari imetoa mwongozo rasmi unaoelekeza namna ya kuratibu maadhimisho hayo katika ngazi zote, ambapo kwa mwaka huu, utekelezaji wake umejikita zaidi katika ngazi ya mikoa ili kuhakikisha ushiriki mpana wa wananchi.

Kwa Mkoa wa Singida, maandalizi yalianza rasmi tangu tarehe 21 Februari 2026 katika ngazi za vijiji na kata, na yanaendelea katika ngazi mbalimbali hadi kufikia kilele cha maadhimisho kitakachofanyika tarehe 7 Machi 2026.

Kaulimbiu ya Maadhimisho Mwaka 2026
yaliongozwa na kaulimbiu isemayo:
**"Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana ni Msingi Jumuishi kufikia Dira ya Taifa ya 2050."**

RC Dendego alisisitiza kuwa kaulimbiu hii inalenga kuhamasisha jamii kutambua mchango wa wanawake katika maendeleo ya taifa, pamoja na kuhimiza ushiriki jumuishi wa wanawake na

wanaume katika kufikia malengo ya muda mrefu ya maendeleo ya nchi.

**Mkakati wa Utekelezaji wa Maadhimisho**
Mkoa wa Singida umeandaa mkakati mahsusi wa utekelezaji wa maadhimisho haya unaolenga kuwafikia wananchi kwa upana zaidi, hususan wanawake walioko katika maeneo ya vijijini.

**Makongamano ya Wilaya:** Kuanzia tarehe 1 Machi 2026, makongamano yatafanyika katika wilaya zote tano za mkoa, yakilenga kutoa elimu na uhamasishaji kuhusu:

**Ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi:** Masuala ya kijamii na kisiasa, Uelewa wa haki na fursa zilizopo, Shughuli za Kijamii na Michezo, Mkoa pia uliandaa bonanza za michezo zitakazoshirikisha makundi mbalimbali ya jamii, ikiwa ni njia ya kuimarisha mshikamano na kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa siku hii.

**Maonyesho ya Wajasiriamali Wanawake:**
Wanawake wajasiriamali watapata fursa ya kuonesha bidhaa na huduma zao, hatua inayolenga kuwapatia jukwaa la kibiashara na kukuza uchumi wao.

**Huduma za Kijamii na Kisheria:** Kutakuwa na utoaji wa huduma mbalimbali, ikiwemo: Ushauri wa kisheria bure, Elimu ya haki za wanawake, Huduma za kijamii kwa makundi maalum.

**Ubunifu wa Maadhimisho ya Mwaka 2026:**
Katika kuboresha ushiriki na ufanisi wa maadhimisho, Mkoa umeanzisha mbinu mpya ya kusogeza huduma karibu na wananchi badala ya wananchi kufuata huduma hizo.

Tofauti na miaka ya nyuma, maadhimisho ya mwaka 2026: Yamepanuliwa kwa muda mrefu zaidi, Yanafanyika katika ngazi zote kuanzia vijiji hadi mkoa, Yanalenga kuwafikia wananchi wengi zaidi, hususan wanawake wa kawaida.

Aidha, mkazo maalum umewekwa katika kuwafikia wanawake wenye ulemavu ili kuhakikisha ushiriki wao unakuwa jumuishi na wenye tija.

RC Dendego bainihs kuwa Kilele cha maadhimisho kitafanyika katika Viwanja vya Lulumba, Wilaya ya Iramba, tarehe 7 Machi 2026. Katika kipindi hicho, shughuli mbalimbali zitafanyika, ikiwa ni pamoja na uzinduzi rasmi wa maadhimisho pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Wananchi watapata fursa ya kupatiwa huduma kutoka taasisi mbalimbali, zikiwemo: Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) – huduma za vitambulisho, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) vyeti vya kuzaliwa, Taasisi za kifedha na mabenki – huduma za kifedha, Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote – elimu na usajili, Watoa huduma za msaada wa kisheria – huduma bure

Huduma hizi zinalenga kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu kwa wananchi katika eneo moja.

**Mgeni Rasmi wa Kilele**
Mkoa wa Singida unatarajia kupokea mgeni rasmi wa heshima katika kilele cha maadhimisho: **Mama Salma Kikwete,** Mke wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne. Ugeni huu unatarajiwa kuongeza uzito wa maadhimisho na kutoa hamasa kwa wananchi kushiriki kikamilifu.

RC Dendego alitoa wito kwa wanawake wa Mkoa wa Singida kujitokeza kwa wingi kushiriki katika maadhimisho haya katika ngazi zote.

Aidha, alihimiza ushiriki wa wanaume na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kuhakikisha malengo ya maadhimisho yanafikiwa kwa ufanisi.

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka 2026 katika Mkoa wa Singida yanadhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake.

Kupitia mkakati jumuishi unaojumuisha utoaji wa elimu, huduma na fursa mbalimbali, Mkoa umeweka msingi imara wa kuhakikisha kuwa wanawake wanapata nafasi stahiki katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Maadhimisho haya si tukio la siku moja, bali ni mchakato endelevu unaolenga kujenga jamii yenye usawa, haki na maendeleo kwa wote.



# Sauti ya Mwanamke wa Singida: Safari ya Mabadiliko Inaendelea

## MANYONI KUFUNGUA MAKONGAMANO YA WANAWAKE NGAZI YA WILAYA




*Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, akitoa hotuba kwa wanawake waliohudhulia kwenye kongamano la Wanawake Wilaya ya Manyoni katika ukumbi wa Halmashauri ikiwa ni shughuli muhimu kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ngazi ya Mkoa.* | PICHA: GCU RS SINGIDA

1 Machi 2026

**Wanawake, Usawa na Dira ya Taifa 2050**

**Sauti ya Mwanamke wa Singida: Safari ya Mabadiliko Inaendelea:**

Katika anga la joto la Wilaya ya Manyoni, siku ya tarehe 1 Machi 2026 haikuwa ya kawaida. Ilikuwa siku ambayo sauti za wanawake zilikutana, ndoto zikapewa mwelekeo, na dira ya maendeleo ya taifa ikawekwa mezani kwa mtazamo mpya, mtazamo unaomweka mwanamke katikati ya maendeleo.

Kongamano la Wanawake lililofanyika mkoani Singida limekuwa jukwaa muhimu la mjadala, tafakari na maamuzi, likikusanya viongozi, wataalamu na wanawake kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa huu wenye historia ya ustahimilivu na ari ya maendeleo.

**Uongozi wa Mkoa: Mwanamke Kama Nguzo ya Maendeleo:**

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, alitoa ujumbe mzito uliogusa kiini cha maendeleo ya taifa. Kwa msisitizo mkubwa, alieleza kuwa uwezeshaji wa wanawake si chaguo bali ni lazima ikiwa taifa linataka kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2050.

Alisisitiza kuwa wanawake wanapaswa kupewa nafasi sawa katika elimu, uchumi na jamii kwa ujumla, akibainisha kuwa usawa wa kijinsia ni msingi wa kujenga taifa lenye haki, ustawi na uchumi imara.

Katika hotuba yake, aligusia pia umuhimu wa




elimu kwa mtoto wa kike—akieleza kuwa elimu hiyo si tu inabadilisha maisha ya mtu mmoja bali ina athari pana kwa jamii nzima kwa kuzalisha viongozi bora, wataalamu mahiri na wananchi wenye uwajibikaji.

**Jukwaa la Fikra:**
**Wanawake Kujadili Mustakabali Wao**



Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt. Fatuma Mganga, alieleza kuwa makongamano ya wanawake ni zaidi ya mikutano—ni majukwaa ya kubadilishana uzoefu, kutathmini mafanikio na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo.

Alisisitiza umuhimu wa mshikamano na uongozi wa wanawake, akieleza kuwa maendeleo hayawezi kupatikana bila umoja na dira ya pamoja. Aidha, kongamano hilo limeweka msingi wa kujadili mada za kitaalamu zitakazowawezesha wanawake kukabiliana na changamoto za kila siku kwa ufanisi zaidi.

**Nguvu ya Kiuchumi:**
**Wanawake Wakijengewa Msingi Imara**

Moja ya mafanikio yaliyoangaziwa kwa fahari katika kongamano hilo ni juhudi za Wilaya ya Manyoni katika kuwawezesha wanawake kiuchumi. Zaidi ya vikundi 113 vya wanawake vimepatiwa mikopo inayozidi shilingi milioni 686, ikiwa ni hatua madhubuti ya kuinua kipato cha kaya na kuchochea uchumi wa mkoa.

Hii si takwimu tu—ni simulizi ya wanawake 991 wanaopata fursa ya kubadili maisha yao, kuanzisha biashara, kuongeza uzalishaji na kushiriki kikamilifu katika uchumi wa ndani.

Kwa lugha ya magazeti, hii ni "mapinduzi ya kimya kimya" yanayofanyika katika ngazi ya jamii.

**Nishati Safi: Fursa Mpya kwa Wanawake**



Katika sura nyingine ya maendeleo, Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dkt. Vicent Mashinji, alizungumzia juhudi za serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi, salama na nafuu kwa wananchi.

Alibainisha kuwa lengo ni kufikia angalau asilimia 80 ya matumizi ya nishati safi ifikapo mwaka







2034—hatua ambayo si tu inalinda mazingira bali pia inaboresha afya za jamii.

Katika muktadha huu, wanawake wamepewa nafasi ya kipekee kama mabalozi wa mabadiliko—kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala majumbani na katika shughuli za uzalishaji. Hapa ndipo mwanamke anapogeuka kuwa kiungo muhimu kati ya sera na utekelezaji wake katika jamii.

Kongamano hili limekuwa sehemu ya maandalizi ya kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, ambapo kwa Mkoa wa Singida sherehe hizo zinatarajiwa kufanyika katika viwanja vya Viwanja vya Lumumba.

Kaulimbiu ya mwaka huu—"Haki na usawa kwa wanawake na wasichana: Msingi jumuishi kufikia Dira 2050"—inaakisi dhamira ya dhati ya kuhakikisha hakuna mwanamke au msichana anayeachwa nyuma katika safari ya maendeleo.

Kongamano la Wanawake Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni halikuwa tu tukio, limekuwa chachu ya mabadiliko. Ni mwanzo wa safari mpya ambapo wanawake wanachukua nafasi yao stahiki katika ujenzi wa taifa.

"Uwezeshaji wa mwanamke ni uwekezaji wa taifa."






# Wanawake ni Nguzo ya Uchumi wa Kisasa wa taifa:

## IKUNGI YAWASHA MOTO WA DIRA YA TAIFA YA 2050, MAKUZI NA MALEZI NYENZO MUHUMU KWA MWANAMKE



*Wanawake wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi wakiwa katika Ukumbi wa Halmashauri wakati wa Kongamano la Wanawake lilifunguliwa rasmi na Mkuu wa Mko wa Singida, Mhe. Halima Dendego kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.* | PICHA: GCU RS SINGIDA

**2 Machi 2026**

Katika harakati za kuelekea Siku ya Wanawake Duniani, Wilaya ya Ikungi imeandika historia mpya kupitia Kongamano la Wanawake lililolenga kuimarisha nafasi ya mwanamke katika safari ya kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Kongamano hilo limefunguliwa rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ambaye alitoa msisitizo mzito juu ya usawa wa kijinsia kama msingi wa maendeleo jumuishi.

"Hakuna Anayepaswa Kuachwa Nyuma"
Katika hotuba yake, Mhe. Dendego alisisitiza kuwa safari ya maendeleo kuelekea mwaka 2050 inahitaji ushiriki wa kila mwananchi, huku akibainisha kuwa mwanamke ana nafasi ya kipekee katika kuchochea ukuaji wa uchumi.

Alimwelezea mwanamke kama injini ya uchumi, akihimiza wanawake kujipanga na kushiriki kikamilifu katika uchumi wa viwanda na biashara za kisasa—hasa katika mifumo ya kidijitali inayokua kwa kasi duniani.

Teknolojia: Fursa na Changamoto kwa Mwanamke
Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya elimu, Mhe. Dendego alieleza kuwa bado kuna pengo la teknolojia linalowakabili wanawake wengi. Alisisitiza umuhimu wa uwekezaji katika ujuzi wa kidijitali ili kuhakikisha wanawake hawabaki nyuma katika mapinduzi ya uchumi wa kisasa.

Amengeza kuwa mwanamke wa leo anapaswa kuwa tayari kutumia teknolojia kama nyenzo ya kukuza biashara, kuongeza kipato na kushiriki katika masoko mapana zaidi.



**Mapambano Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia**
Kongamano hilo pia limeweka msisitizo katika kupinga ukatili wa kijinsia, likitambua kuwa maendeleo hayawezi kupatikana bila mazingira salama na yenye usawa kwa wanawake.

Mhe. Dendego alihimiza mshikamano wa kifamilia na ushirikiano kati ya wanawake na wanaume kama njia ya kujenga jamii imara na yenye heshima.

**Maadili: Nguzo ya Maendeleo Endelevu:**
Akichangia mada ya malezi na makuzi, Katibu Tawala Mkoa wa SIngida, Dkt. Fatuma Mganga alieleza kuwa maadili ni uti wa mgongo wa familia na jamii.



Alionya kuwa mmomonyoko wa maadili unaweza kudhoofisha ustawi wa kizazi na kuathiri maendeleo ya taifa. Kwa msisitizo, alitaja uaminifu, nidhamu na uwajibikaji kama misingi muhimu ya mafanikio ya mtu binafsi na jamii kwa ujumla.



Aliongeza kuwa katika dunia ya leo, maadili yanaweza kuwa na uzito mkubwa kuliko hata vyeti katika ajira na maendeleo.

**Majadiliano Yenye Mwelekeo wa Baadaye:**
Kongamano hilo limejadili mada mbalimbali zenye mwelekeo wa maendeleo ya kisasa, ikiwemo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Msaada wa kisheria Bima ya Afya kwa Wote, Matumizi ya Nishati safi, Biashara na uwekezaji na Mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia

Kupitia mada hizi, wanawake wamepata uelewa mpana wa nafasi yao katika kujenga uchumi imara na jamii yenye ustawi.

**Mwanamke wa Leo, Taifa la Kesho:**
Kongamano la Ikungi limeacha alama ya matumaini na mwelekeo mpya. Ujumbe wake ni wazi: Mwanamke akishirikishwa kikamilifu, Dira ya 2050 si ndoto ni uhalisia unaowezekana.
Wanawake wa Ikungi walionesha kuwa wako tayari sio tu kushiriki, bali kuongoza katika safari ya maendeleo ya kisasa.

WATOA MAADA MBALIMBALI KATIKA KONGAMANO LA WANAWAKE HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI














# Malezi, Maadili na Mustakabali wa Jamii

## WILAYA YA SINGIDA YAJENGA KESHO: WANAWAKE WAPEWA JUKUMU LA KUKUZA MAADILI NA MALEZI BORA



*Wanawake mbalimbali wa Wilaya ya Singida wakiwa katika Ukumbi wa Social Mabula Manispaa ya Singida wakati wa Kongamano la Wanawake lilifunguliwa rasmi na Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini, Mhe. Yagi Kiaratu kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.* | PICHA: GCU RS SINGIDA

**3 Machi 2026**

Kongamano la Wanawake wa Wilaya ya Singida, lililofanyika tarehe 3 Machi 2026 kama sehemu ya maandalizi ya Siku ya Wanawake Duniani, limeibua mjadala muhimu kuhusu nafasi ya maadili na malezi katika maendeleo ya jamii.

Katika kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka 2026, Mkoa wa Singida umeendelea kuonesha dhamira ya dhati katika kuimarisha nafasi ya mwanamke kupitia majukwaa ya majadiliano, elimu na utambuzi wa mchango wa wanawake katika jamii.

Moja ya matukio muhimu katika mfululizo huo ni Kongamano la Wanawake wa Wilaya ya Singida lililofanyika tarehe 3 Machi 2026 katika Ukumbi wa Social Mabula, Manispaa ya Singida. Kongamano hilo limewakutanisha wanawake kutoka maeneo mbalimbali kwa lengo la kujadili masuala ya usawa wa kijinsia, maadili, malezi na uwezeshaji wa wanawake katika nyanja za maendeleo.

**Wito wa Hatua za Vitendo katika Usawa wa Kijinsia:**

Akizungumza katika kongamano hilo, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini, Mhe. Yagi Kiaratu, aliwataka wanawake kuhamia katika utekelezaji wa vitendo vya usawa wa kijinsia badala ya kuishia katika mijadala ya maneno.




Alieleza kuwa, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha nafasi ya mwanamke, bado kuna haja ya kuongeza juhudi ili kufikia usawa kamili katika nyanja zote za maendeleo.

"Tumepiga hatua kubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Hata hivyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa mwanamke anapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika uchumi, kumiliki mali, na kuwa

na mamlaka ya kuitumia mali hiyo kwa manufaa yake na ya jamii," alisisitiza.

Aidha, alielekeza mkazo katika umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike, akibainisha kuwa elimu ni msingi wa kumwezesha mwanamke kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa.

"Mtoto wa kike ana haki ya kupata elimu. Kupitia elimu, anawezeshwa kujenga maisha yake na kutoa mchango mkubwa katika jamii," aliongeza.

**Serikali Kuimarisha Huduma za Afya kwa Wanawake:**
Katika muktadha wa uwezeshaji wa wanawake, Mhe. Kiaratu alieleza juhudi zinazoendelea kufanywa na Serikali katika kuboresha huduma za afya, hususan afya ya uzazi.

Alibainisha kuwa utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote unaendelea kuwa chombo muhimu katika kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote.

"Mpango huu unahakikisha mwananchi anapata huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za rufaa. Hii ni hatua muhimu katika kulinda afya ya mama na mtoto," alieleza.

**Maadili na Malezi: Msingi wa Jamii Endelevu:**
Sambamba na masuala ya usawa na uwezeshaji, kongamano hilo lilitoa nafasi ya kujadili umuhimu wa maadili na malezi bora katika kujenga jamii yenye ustawi.

Akiwasilisha mada hiyo, Bi. Joanfaith Kataraia alisisitiza kuwa maadili ni msingi wa maisha ya kijamii na kwamba malezi bora yanaanza ndani ya familia, ambapo wanawake wanabeba jukumu kubwa la kuhakikisha tunu hizo zinadumishwa.



Alieleza kuwa maadili hujidhihirisha kupitia matendo ya kila siku, hususan katika namna mtu anavyotekeleza majukumu yake kwa bidii, uwajibikaji na uadilifu.

"Mtu mwenye maadili hutambuliwa kwa namna anavyofanya kazi kwa bidii, kuheshimu muda na kuepuka uzembe au visingizio visivyo na msingi," alifafanua.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa haki na usawa katika mahusiano ya kijamii, akibainisha kuwa kuheshimiana na kutendeana haki ni nguzo muhimu ya maadili mema.

**Utambuzi wa Wanawake Vinara wa Maendeleo:**
Katika kuhitimisha kongamano hilo, wanawake sita walitambuliwa na kupongezwa kwa mchango wao katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya jamii, hatua iliyolenga kuhamasisha wanawake wengine kuiga mifano bora ya mafanikio.



Washindi hao walikabidhiwa zawadi ya mitungi ya gesi ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi na salama.

Utambuzi huu umebeba ujumbe mpana wa kuthamini juhudi za wanawake na kuhamasisha matumizi ya nishati safi, ambayo ni muhimu kwa afya ya familia na uhifadhi wa mazingira.

**Biashara ya Leo Inahitaji Ubunifu wa Kesho**
Akiwasilisha mada kuhusu uwekezaji na fursa za kiuchumi, Bi. Happiness Rugeimukamu alisisitiza kuwa wanawake wanapaswa kujitofautisha katika biashara wanazozifanya.

Alieleza kuwa katika dunia ya leo, kufanya biashara pekee haitoshi ni lazima mfanyabiashara awe na ubunifu katika bidhaa au huduma anazotoa ili

kuvutia wateja na kuhimili ushindani.



Kwa mtazamo wake, ubunifu ni daraja linalounganisha biashara ndogo na mafanikio makubwa.

**Kujiamini ni n**guvu ya Ndani ya Mfanyabiashara. Mbali na ubunifu, alisisitiza umuhimu wa kujiamini kwa wanawake wanaojishughulisha na biashara. Alieleza kuwa hofu na mashaka vinaweza kuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo ya biashara.

Kwa maneno yake, mfanyabiashara anayejithamini na kujiamini ana nafasi kubwa ya kukua na kufikia mafanikio ya muda mrefu.

**Fursa Zipo Ni Kuzitumia Tu**

Katika kongamano hilo, wanawake walikumbushwa kuwa fursa za kiuchumi zipo nyingi kutoka mikopo ya halmashauri hadi masoko ya ndani na nje ya mkoa. Hata hivyo, mafanikio yanategemea namna wanavyotumia fursa hizo kwa ubunifu na ufanisi.

Bi. Rugeimukamu alibainisha kuwa wanawake wana uwezo mkubwa wa kuwekeza na kukuza biashara zao endapo wataamua kutumia vizuri rasilimali walizonazo pamoja na maarifa wanayopata.

**Kongamano Kama Jukwaa na Chachu ya Mabadiliko ya Kiuchumi:**

Kupitia majukwaa haya, wanawake wanapata fursa ya kujengewa uelewa kuhusu haki zao, kushirikiana katika kujadili changamoto na kuhamasishwa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kupitia kongamano hili, wanawake wamepata fursa ya kubadilishana uzoefu, kujifunza na kujengewa uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**Mwanamke Mbunifu, Biashara Imara:**

Mkoani Singida, hadithi ya mwanamke mfanyabiashara inaandikwa upya kwa ubunifu, ujasiri na maono mapya.

Kongamano hilo lilibeba ujumbe unaojumuisha utekelezaji wa usawa wa kijinsia kwa vitendo, umuhimu wa maadili na malezi bora, pamoja na kutambua mchango wa wanawake katika jamii. Na Ujumbe wa kongamano hili unabaki kuwa; Tofauti yako ndiyo nguvu yako na ubunifu wako ndiyo tiketi ya mafanikio.


































# Mwanamke Hasubiri Tena, Anachukua Hatua thabiti kufikia malengo yake!

## MKALAMA YATANGAZA ENZI MPYA




*Wanawake wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama wakiwa katika Ukumbi wa Halmashauri wakati wa Kongamano la Wanawake lililofunguliwa rasmi na Mkuu wa Mko wa Singida, Mhe. Halima Dendego kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.* | PICHA: GCU RS SINGIDA

**4 Machi 2026**

Katika Wilaya ya Mkalama, kulisikika sauti moja yenye nguvu sauti ya mabadiliko. Wanawake walikusanyika kwa lengo moja kuu: kuthibitisha kuwa wakati wa kubaki nyuma umefika mwisho, na sasa ni muda wa kusonga mbele kwa ujasiri na maamuzi thabiti.

Kongamano la Wanawake wa Wilaya ya Mkalama, lililofanyika kuelekea Siku ya Wanawake Duniani, limebeba ujumbe mzito wa kuamsha ari, kujenga uwezo na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya jamii.

### Kauli Thabiti ya Uongozi: Mwanamke Asibaki Nyuma

Akizungumza katika kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe., Halima Dendego, alitoa kauli iliyojaa msisitizo na matumaini kuwa zama za mwanamke kubaki nyuma zimekwisha.

Aliwataka wanawake kushiriki kikamilifu katika maamuzi ya familia na taifa, akieleza kuwa maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana bila ushiriki wao katika nyanja zote—kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kwa sauti ya kuhamasisha, aliwahimiza wanawake kujithamini, kutumia fursa zinazotolewa na serikali na kushirikiana na wanaume katika kujenga jamii imara inayolenga kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.



**Malezi Bora: Mbegu ya Jamii Yenye Maadili**
Katika mjadala wa kina kuhusu jamii na mustakabali wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt. Fatuma Mganga, alisisitiza umuhimu wa malezi bora kwa watoto.



Alieleza kuwa wazazi wanapaswa kuwalea watoto katika misingi ya kazi, uwajibikaji na nidhamu tangu wakiwa wadogo, badala ya kuwazoesha kutegemea zawadi au vishawishi ili watimize wajibu wao.

Kwa mtazamo wake, malezi bora ndiyo msingi wa kujenga kizazi chenye uadilifu na jamii yenye heshima.

**Mafanikio Yanayoonekana:** Kongamano hili halikubeba maneno pekee, bali pia lilionesha matokeo halisi ya juhudi za maendeleo. Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Moses: Wanawake wamewezeshwa mikopo ya shilingi milioni 145, Zaidi ya wanawake 500 walishiriki kongamano, Shilingi milioni 3 zimekusanywa kusaidia watoto wenye mahitaji maalum, na Zaidi ya miti 200 imepandwa tangu Machi 2021.

Hizi ni ishara za mabadiliko yanayoonekana mabadiliko yanayoanzia kwa mwanamke mmoja hadi jamii nzima.

**Haki na Uelewa: Sheria Kuwafikia Wanawake:**
Kupitia kampeni ya msaada wa kisheria, wanawake wa Mkalama wamepata fursa ya kujifunza haki zao na kupata msaada wa kisheria bila malipo. Hii imeongeza uelewa wao kuhusu sheria na kuwapa nguvu ya kujilinda na kudai haki zao katika jamii.



**Wanawake Wazungumza: Maarifa Yawapa Nguvu Mpya**
Washiriki wa kongamano hilo walieleza kuwa elimu waliyoipata imewapa mwanga mpya katika maisha yao. Wameahidi kutumia maarifa hayo kuboresha malezi ya watoto, kujitegemea kiuchumi na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Mkalama na taifa kwa ujumla.

**Mwanamke Akiamka, Dunia Hubadilika**
Mkalama imeandika ukurasa mpya—ukurasa unaoonesha mwanamke asiye na woga, mwenye maono na aliye tayari kuchukua nafasi yake katika maendeleo.

**Ujumbe ni wazi:** Mwanamke wa leo hasubiri tena anachukua hatua, anaongoza na anabadilisha dunia yake.






FIKIA DIRA 2050"
chi, 2026
KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 2026

# Mwanamke: Jasiri, Mwenye Maono na Tayari kwa Mafanikio

## UWEZESHAJI, UTHUBUTU NA SAFARI YA MAFANIKIO YA WANAWAKE WA SINGIDA



*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lulumba wakitumbuiza mbele ya Wanawake wa wilaya ya Iramba katika Ukumbi wa Halmashauri wakati wa Kongamano la Wanawake lilifunguliwa rasmi na Mkuu wa Mko wa Singida, Mhe. Halima Dendego kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.*
| PICHA: GCU RS SINGIDA

**5 Machi 2026**

Iramba Yasikika kwa Sauti ya Mwanamke mwenye ujasiri, Mwenye Maono na Tayari kwa Mafanikio: Katika ardhi ya Iramba, ambapo upepo wa mabadiliko unaanza kuvuma kwa nguvu mpya, wanawake walikusanyika si kwa kawaida bali kwa dhamira ya kujenga kesho iliyo bora zaidi. Kongamano la Wanawake wa Wilaya ya Iramba limegeuka kuwa zaidi ya mkutano; limekuwa ni jukwaa la kuamsha ujasiri, kujitambua na kuchukua hatua.

Ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Siku ya Wanawake Duniani, tukio hili limebeba ujumbe mzito: mwanamke anaweza, anastahili na anapaswa kufanikiwa.

**Ujumbe wa Uthubutu:**
Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, alitoa wito wa kipekee kwa wanawake kuwa na ujasiri, kufanya kazi kwa bidii na kujiamini katika safari yao ya maendeleo.

Kwa msisitizo, aliwakumbusha kuwa makongamano kama haya si sehemu ya kusikiliza tu, bali ni fursa ya kujifunza, kuunganika na hatimaye kufikia ndoto zao.

Alieleza wazi kuwa wanawake ni nguzo muhimu ya maendeleo ya taifa na familia, na kwamba mafanikio makubwa yanayoonekana nchini ni ushahidi wa uwezo wao katika uongozi na katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya jamii.



**Fursa za Kiuchumi: Mikopo Kama Chachu ya Mabadiliko.**
Katika kuimarisha uchumi wa wanawake, RC Dendego alisisitiza umuhimu wa kuongeza kasi ya kuwafikia wanawake wote walioko kwenye vikundi ili waweze kunufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri.

Hii ni zaidi ya fedha ni mlango wa fursa. Ni mwanzo wa safari ya kujitegemea, kuanzisha biashara, kukuza kipato na hatimaye kubadilisha maisha ya familia na jamii kwa ujumla.

**Malezi na Maadili: Msingi wa Jamii Imara.**
Katika kongamano hilo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt. Fatuma Mganga, aliwasilisha mada muhimu kuhusu makuzi, malezi na ukatili wa kijinsia.



Dkt. Mganga alieleza kuwa ukosefu wa maadili katika jamii ni chanzo kikubwa cha migogoro na vitendo vya unyanyasaji. Alisisitiza wajibu wa wazazi katika kulea watoto kwa misingi ya nidhamu, uwajibikaji na heshima—misingi itakayojenga jamii yenye amani na mshikamano.

Aidha, aliwahimiza wanawake kujenga uchumi imara ili kuimarisha familia na kuchangia ustawi wa jamii kwa upana zaidi.

Maarifa kwa Maendeleo: Mada Zilizogusa Maisha Halisi
Kongamano hilo halikuishia kwenye hotuba pekee. Washiriki walipata fursa ya kujifunza kupitia mada mbalimbali zilizolenga maisha yao ya kila siku:

Nishati Safi: Iliyowasilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleimani Mwenda, ikielekeza matumizi ya nishati mbadala kwa afya na mazingira bora

**Uchumi na Uwekezaji:**
Mada Iliyowasilishwa na Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Bishara, Viwanda na Uwekezaji, Bi. Donatila Vedasto, alitwaasa wanawake kuziona fursa kwa kuifungua milango ya fikra mpya za biashara na uwekezaji.



**Elimu ya Sheria: I**liyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Sheria Mkoa wa Singida Bi. Matrida Nickson, ikihusisha kampeni ya msaada wa kisheria kwa wananchi ili kuepuka ulaghai wanaopitia wanawake katika nyanja mbalimbali.

**Mada hizi na nyinginezo zilizotolewa katika kongamano hilo zilibeba ujumbe mmoja mkuu maarifa ni nguvu, na mwanamke mwenye maarifa ana uwezo wa kubadilisha dunia yake.**

**Sauti za Wanawake: Maarifa Yaleta Mabadiliko**
Baada ya kongamano, baadhi ya wanawake walioshiriki walieleza kufurahishwa na elimu waliyoipata. Walibainisha kuwa wamepata uelewa mpana kuhusu masuala ya uchumi, malezi, sheria na maendeleo ya mwanamke.

Kwao, kongamano hili halikuwa mwisho—bali mwanzo wa safari mpya ya kuboresha maisha yao na kuchangia maendeleo ya familia na jamii.

**"Mwanamke Akiaminiwa, Jamii Inainuka"**
Iramba imeonyesha mfano kwamba pale mwanamke anapopewa nafasi, maarifa na fursa, anaweza kufanya makubwa.

Kongamano hili limeacha alama ya kudumu kwa kuonesha kuwa kujiamini kwa mwanamke ni mwanzo wa mafanikio, na fursa zikitumika ipasavyo, mabadiliko huwa ya hakika.




















JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA
KONGAMANO LA WANAWAKE
TAREHE 05/03/2026
MGENI RASMI
MHE. HALIMA DENDEGO
MKUU WA MKOA WA SINGIDA
UKUMBI MKUBWA WA HALMASHAURI YA
WILAYA YA IRAMBA
"Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana:
Msingi Jumuishi Kufikia Dira 2050"

# "Malezi bora, maadili imara"

## WITO WA MAMA SALMA KIKWETE, WANAWAKE VINARA WATAMBULIWA KWA MAFANIKIO YAO



*Mhe. Salma Kikwete (Mb) Mke wa Rais Mstaafu awamu ya nne akihutubia Wanawake na Wananchi katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ngazi ya Mkoa katika Viwanja vya Lulumba Wilay ya Iramba Mkoani Singida .* | PICHA: GCU RS SINGIDA

**7 Machi 2026**

Maelfu ya wanawake pamoja na wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Singida walikusanyika katika Viwanja vya CCM Lulumba, Wilaya ya Iramba, kushiriki kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ngazi ya mkoa, yaliyofanyika tarehe 7 Machi 2026 kwa mafanikio makubwa.

Maadhimisho hayo yalikuwa jukwaa la kuenzi mchango wa wanawake katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, sambamba na kuhamasisha usawa wa kijinsia, mshikamano na uwezeshaji wa wanawake katika nyanja zote za maisha.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa Mbunge wa Jimbo la Mchinga na Mke wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, ambaye aliongoza shughuli hizo na kutoa ujumbe mzito kwa wanawake na jamii kwa ujumla.

**Wito wa Malezi Bora na Maadili ya Jamii:**
Akizungumza katika kilele cha maadhimisho hayo, Mhe. Salma Kikwete aliwahimiza wanawake nchini kuwekeza nguvu zaidi katika malezi bora ya watoto ili kujenga jamii yenye maadili mema na ustawi wa kudumu.

Alisisitiza kuwa wanawake wanayo nafasi ya kipekee katika malezi ya watoto, na kwamba jukumu hilo linapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia misingi ya maadili na tamaduni nzuri za Kitanzania.

"Wanawake tuna jukumu kubwa la kuhakikisha watoto wa kike na wa kiume wanalelewa katika




misingi ya maadili na tamaduni nzuri za Kitanzania," alisema.

Aidha, aliwahimiza wanawake kuendelea kudumisha heshima ndani ya familia, akieleza kuwa familia imara ndiyo msingi wa maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.




"Ni muhimu pia wanawake kuwaheshimu waume zao, kwa kuwa familia yenye mshikamano na heshima ni msingi wa maendeleo endelevu," aliongeza.

**Uwezeshaji wa Wanawake na Fursa za Kiuchumi:** Katika maadhimisho hayo, msisitizo uliwekwa pia katika uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kupitia shughuli za ujasiriamali na ubunifu.

Mhe. Salma Kikwete alipata fursa ya kutembelea mabanda ya wajasiriamali wanawake yaliyokuwa yameandaliwa katika viwanja hivyo, ambapo alijionea na kununua bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na wanawake, ikiwemo asali safi na miiko ya kupikia.

Ziara hiyo ilionesha juhudi na ubunifu wa wanawake wa Singida katika kujikwamua kiuchumi, huku pia ikiakisi fursa zinazotolewa kupitia programu mbalimbali za maendeleo, ikiwemo zile zinazoratibiwa kwa ushirikiano na wadau kama Helvetas.

Ushiriki wa mgeni rasmi katika shughuli hizo uliimarisha hamasa kwa wanawake wajasiriamali na kuonesha umuhimu wa kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika uchumi wa taifa.



**Utambuzi wa Wanawake Vinara wa Maendeleo:** Sehemu muhimu ya maadhimisho hayo ilikuwa ni utoaji wa tuzo na zawadi kwa wanawake waliofanya vizuri katika nyanja mbalimbali, ikiwemo uchumi, ushawishi wa kijamii na malezi bora.

Wanawake vinara kutoka wilaya mbalimbali za Mkoa wa Singida walitambuliwa na kupatiwa zawadi mbalimbali kama sehemu ya kuthamini mchango wao katika maendeleo ya jamii na kuhamasisha wengine kuiga mifano hiyo.

Hatua hii imeendelea kuwa chachu ya kuwahamasisha wanawake kujituma zaidi katika shughuli za maendeleo na kuchangia katika ustawi wa jamii.



**Ushindani wa Wilaya: Singida Yaibuka Kinara:**
Katika ushindani ulioshirikisha wilaya mbalimbali za Mkoa wa Singida, Wilaya ya Singida iliibuka mshindi wa nafasi ya kwanza kufuatia ushiriki wake mzuri katika shughuli na mashindano yaliyoandaliwa wakati wa maadhimisho hayo.

Wilaya ya Mkalama ilishika nafasi ya pili, huku Wilaya ya Iramba ikishika nafasi ya tatu. Nafasi ya nne ilichukuliwa na Wilaya ya Ikungi na nafasi ya tano kwenda Wilaya ya Manyoni.

Matokeo hayo yanaonesha kiwango cha ushiriki, mshikamano na juhudi zinazofanywa na wanawake katika wilaya mbalimbali katika kuendeleza agenda ya maendeleo.



**Maadhimisho Yaliyojaa Shughuli Mbalimbali:**
Mbali na utoaji wa tuzo, maadhimisho hayo yalipambwa na shughuli mbalimbali zilizolenga kuhamasisha na kuelimisha jamii, zikiwemo: Maonesho ya vikundi vya wanawake, Burudani mbalimbali za kijamii, na Majadiliano ya masuala ya maendeleo.

Matukio hayo yalitoa fursa kwa wanawake kubadilishana uzoefu, kujifunza na kuimarisha mshikamano wao katika kujenga jamii bora.



**Utambuzi wa Wanawake Vinara wa Maendeleo:**
Wanawake vinara kutoka wilaya mbalimbali za Mkoa wa Singida walitambuliwa na kupatiwa zawadi mbalimbali kama sehemu ya kuthamini mchango wao katika maendeleo ya jamii na kuhamasisha wengine kuiga mifano hiyo.

Hatua hii imeendelea kuwa chachu ya kuwahamasisha wanawake kujituma zaidi katika shughuli za maendeleo na kuchangia katika ustawi wa jamii.



**Salamu za Shukrani kwa Mgeni Rasmi:**
Katika kuhitimisha maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Yusuph Mwenda, aliwasilisha salamu za shukrani kwa mgeni rasmi kwa kukubali kushiriki na kuongoza tukio hilo muhimu.

Alieleza kuwa uwepo wa Mheshimiwa Salma Kikwete umeongeza thamani ya maadhimisho hayo na kutoa hamasa kwa wanawake wa Mkoa wa Singida kuendelea kushiriki katika maendeleo ya jamii.

Aidha, alibainisha kuwa maadhimisho hayo yamefanikiwa kuwaunganisha wanawake kutoka wilaya mbalimbali na kuimarisha mshikamano wao katika kuendeleza ajenda ya usawa wa kijinsia na maendeleo endelevu.

**Mwanamke ni Nguzo ya Maendeleo:**
Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka 2026 katika Mkoa wa Singida yameacha ujumbe mzito kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii—kuanzia malezi, uchumi hadi uongozi.

Kupitia wito wa malezi bora, uwezeshaji wa kiuchumi na utambuzi wa mafanikio, imebainika wazi kuwa mwanamke ana nafasi ya kipekee katika kujenga jamii yenye maadili, mshikamano na maendeleo endelevu.

Kadri Mkoa wa Singida unavyoendelea kuimarisha juhudi hizi, maadhimisho haya yanabaki kuwa si tukio la siku moja, bali ni chachu ya mabadiliko ya kudumu katika jamii.

# HABARI PICHA YA MATUKIO MBALIMBALI













HONGERA DKT. SAMIA KWA KUPIGANIA MASLAHI YA WANAWAKE NCHINI
SIKU YA WANAWAKE MKOA - SINGIDA
07.03.2026




HAKI KWA WANAWAKE NA WASICHANA,
MSINGI WA MAENDELEO JUMUISHI
KUFIKIA DIRA 2050."


JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI MKOA WA SINGIDA
SIKU YA WANAWAKE DUNIANI










SIKU YA WANAWAKE 2026




















SIKU YA WANAWAKE DUNIANI


HONGERA DKT. SAMIA KWA KUPIGANIA
MASLAHI YA WANAWAKE NCHINI


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HONGERA DKT. SAMIA KWA KUPIGANIA
MASLAHI YA WANAWAKE NCHINI
"Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana:
Msingi jumuishi kufikia Dira 2050"


HONGERA DKT. SAMIA KWA KUPIGANIA
MASLAHI YA WANAWAKE NCHINI






SIKU YA WANAWAKE
MKOA - SINGIDA - 2026
AQUALUNG




JAMHURI YA


JAMHURI YA
MUUNGANO WA
TANZANIA


MUUNGANO WA


JAMHURI YA


TUZO YA HESHIMA










SIKU YA WANAWAKE MKOA - SINGIDA - 2026



ZAWADI KUTOKA SINGIDA




































JAMHURI YA
MUUNGANO WA
TANZANIA

# Matendo ya Huruma

## WANAWAKE WA SINGIDA WAGUSA MAISHA YA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM




*Mhe. Salma Kikwete (Mb) Mke wa Rais Mstaafu awamu ya nne akihutubia Wanawake na Wananchi katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ngazi ya Mkoa katika Viwanja vya Lulumba Wilay ya Iramba Mkoani Singida .* | PICHA: GCU RS SINGIDA

**8 Machi 2026**

Moyo wa Huruma: Wanawake wa Singida Wagusa Maisha ya Watoto Wenye Mahitaji Maalum Katika kijiji cha Kizega, kilichojaa utulivu wa vijijini lakini pia changamoto za maisha, kulishuhudiwa tukio lililobeba uzito wa upendo, mshikamano na matumaini. Siku hiyo haikuwa ya kawaida kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kizega—ilikuwa ni siku ambayo waliona kwa vitendo maana halisi ya jamii inayojali.

Ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Siku ya Wanawake Duniani, wanawake wa Mkoa wa Singida waliamua kubadili dhana ya maadhimisho—kutoka sherehe za kawaida hadi matendo ya huruma yanayogusa maisha ya wahitaji.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alitoa wito kwa wanawake kutumia sehemu ya rasilimali walizonazo kusaidia makundi yenye uhitaji katika jamii.

Kwa sauti ya huruma na msisitizo, alieleza kuwa nguvu ya mwanamke haipo tu katika kujiletea maendeleo binafsi, bali pia katika kuinua wengine wanaohitaji msaada.

Alisisitiza kuwa maadhimisho haya yanapaswa kuwa na maana pana zaidi—kuwa chachu ya mabadiliko chanya katika jamii.

Zaidi ya Sherehe: Maadhimisho Yenye Maana Halisi
Katika tukio hilo, Kamati ya Maandalizi ya maadhimisho ilifika katika Shule ya Msingi Kizega na kukabidhi msaada kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Msaada huo haukuwa tu vitu—bali ulikuwa ni ishara ya upendo na kujali.

Miongoni mwa vilivyotolewa ni: Kilo 200 za mchele, Kilo 50 za sukari, Sabuni na mafuta ya kupikia, Taulo za kike na Viti mwendo viwili

Hivi vyote vililenga kupunguza changamoto za kila siku wanazokutana nazo wanafunzi hawa, na kuwapa mazingira bora zaidi ya kujifunzia na kuishi.

Viongozi Wanoungana kwa Lengo Moja
Ziara hiyo iliunganisha viongozi mbalimbali wa



wanawake na taasisi kutoka mkoa mzima. Miongoni mwao walikuwepo Katibu Tawala wa Mkoa, Fatuma Mganga, pamoja na viongozi wengine wa vyama na mashirika walioungana kwa lengo moja—kuleta mabadiliko chanya kwa jamii.

Ushiriki wao ulionesha wazi kuwa maendeleo ya jamii yanahitaji mshikamano wa pamoja na dhamira ya kweli.

**Sauti Kutoka Iramba: Faraja kwa Wanafunzi**
Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleimani Mwenda, alieleza kuwa wanafunzi wa shule hiyo wanatoka katika makundi mbalimbali ya wenye mahitaji maalum na wanahitaji uangalizi wa karibu.

Alibainisha kuwa msaada huo si tu unatoa nafuu ya mahitaji ya msingi bali pia unaleta faraja na motisha kwa wanafunzi kuendelea na masomo yao kwa bidii.

**Shukrani Kutoka Shuleni**
Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Elisante Dius, alielezea shukrani zake za dhati kwa msaada uliotolewa. Alisema kuwa mchango huo utasaidia kupunguza baadhi ya changamoto zinazowakabili wanafunzi wenye mahitaji maalum, na hivyo kuboresha mazingira yao ya kujifunzia.

Lakini pengine sauti iliyogusa zaidi ilikuwa ya wanafunzi wenyewe.

Kwa niaba yao, walitoa shukrani kwa wanawake wa Mkoa wa Singida, wakisema msaada huo utawasaidia katika maisha yao ya kila siku na kuwapa moyo mpya wa kuendelea na masomo.

Hitimisho: Matendo Madogo, Athari Kubwa
Katika dunia inayokimbilia maendeleo ya kasi, matendo ya huruma kama haya yanatukumbusha thamani ya ubinadamu. Wanawake wa Singida wameonyesha kuwa maendeleo ya kweli hayaishii kwenye takwimu—bali yanaonekana katika maisha yanayoguswa na kubadilishwa.

Hii ni hadithi ya upendo.
Hii ni hadithi ya matumaini.
Na juu ya yote—hii ni hadithi ya jamii inayojali.





















SINGIDA YETU
NURU YA MAENDELEO
JARIDA MAALUM LA OFISI YA MKUU WA MKOA WA SINGIDA
TOLEO LA MACHI 2026

Jarida Maalum la Maadhimisho ya Siku ya

# Wanawake DUNIANI 2026




**Jarida hili limetolewa na**
**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida**
**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

"Tunachochea Mendeleo, Kupitia Taarifa Sahihi"

**www.singida.go.tz**
barua@singida.go.tz

